**Learning by Ear – Climate Change**

**Episode 04**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

CHARACTERS:

Scene 1:

- JOSHUA (15)
- CAROL (14)
- ALEX (15)
- LORNA (16)

Scene 2:

- DR FENTON (45)
- JOSHUA (15)
- CAROL (14)
- ALEX (15)
- LORNA (16)

Scene 3:

- DR FENTON (45)
- JOSHUA (15)
- CAROL (14)
- ALEX (15)
- LORNA (16

Scene 4:

- CAROL (14)
- PASSER-BY (MALE ADULT)
- HEAVY (MALE ADULT)

**Intro:**

Ni mara nyingine tunapoungana nawe msikilizaki kukuletea makala haya ya “Noa Bongo Jenga Maisha Yako”, kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa. Jopo la kazi kushughulikia suala la mabadiliko ya hali ya hewa tayari limeundwa, japo linakabiliwa na kibarua kigumu endapo linataka kusimamisha mradi wa ujenzi wa kiwanda cha Umeme katika kijiji cha Dhowville. Jopo hilo linahitaji kujihami ipasavyo katika kukabiliana na changamoto hii. Katika kipindi hiki wanafunzi hawa wanne wanakutana na mtaalam wa masuala ya mazingira ambaye

anawafumbua macho kuhusu husiano kati ya mabadiliko ya hali ya hewa na ujenzi wa viwanda. Karibu katikasehemu ya nne.

**Scene One: On the Train to the city**

| | |
|---|---|
| **SFX:** | **DOORS SLAMMING, TRAIN BELL, TRAIN PULLING OUT OF STATION** |
| **SFX ATMO:** | **INSIDE TRAIN** |
| **1. LORNA:** | Sawa, basi sasa tunaweza kuzama katika wingu hili la moshi. Nadhani kila mmoja wetu amebeba kifaa chake cha kuchuja hewa, sivyo! |
| **2. JOSHUA**: | Nini, Lorna? Kifaa cha kuchuja hewa? |
| **3. LORNA:** | Aah ulikuwa mzaha kidogo! Watu husema wanaingia kwenye wingu la moshi wakiwa na maana mji mkubwa kuelezea kuhusu uchafuzi wa mazingira unaoendelea huko. |

**4. CAROL:** Oh….naelewa sasa! Na kweli moshi wote huu,kutoka kwa mabasi,magari madogo viwanda…!

**5. LORNA:** Miji mikubwa kama huu kwa kawaida huwa na idadi kubwa ya watu na wote hao hutumia kiwango kikubwa cha nishati.

**6. ALEX:** Na kwa hivyo, kuna utoaji mkubwa wa gesi za viwandani na mabadiliko mengi zaidi ya hali ya hewa. Ni mzunguko!

**7. JOSHUA:** Hii ni mara yangu ya kwanza kutia guu langu jijini au nisema kuingia katika wingu kubwa la moshi wa aina hii kama mnavyoita. Sijui huyu mwanasayansi wa mazingira anakaa vipi. Na je, hufanya nini?

**8. LORNA:** Sikuwa na uhakika, kwa hivyo nikafanya utafiti katika tovuti ya Google kwenye mtandao wa intaneti katika kompyuta ya mama yangu!

**9. CAROL:** Lilikuwa wazo zuri sana, Lorna.

**10. LORNA:** Niliandika mahali **(opening notebook and reading)** “Mwanasayansi wa mazingira hupima na kurekodi sehemu za mzingira, kutafiti, kufikia na kuvumbua njia za kudhibiti au kupunguza athari hatari zinazosababishwa na shughuli za binadamu katika mazingira na kuanzisha mipango ya kuhifadhi mazingira hayo.

**11. ALEX:** Hiyo ni kazi ya aina gani? Mtu yeyote anaweza kupima na kurekodi hali ya mazingira.

**12. CAROL:** Hilo ni kweli lakini bado sijaelewa…! Nilidhani mtaalam huyu ni mtu anayefanya zaidi ya vile wengine wanavyoweza kufanya, anayefanana na sisi lakini mwenye sifa nzuri zaidi kimasomo.

**13. JOSHUA:** Nafikiri tumefika-, Gari moshi sasa limesimama.

**14. LORNA:** Hebu tumsikilize anasema nini.! tufanyeni haraka , tushuke!.

**(running to get off train)**

**SFX:** **DOORS SLAMMING**

**Scene Two: City Streets**

**SFX ATMO:** **CITY STREET NOISE**

**15. CAROL:** Sasa tunakwenda wapi, Lorna?

**16. LORNA:** Amesema tumsubiri nje karibu na mahala panapoegeshwa teksi, ambapo ni hapa!

**17. DR FENTON:** Habari gani? .Wewe ni Lorna? Na nadhani hawa ni wanachama wenzako katika jopo hili, sivyo?

**18. LORNA:** **W**ewe ni Dkt Fenton? Ndio huyu ni Carol,Joshua na Alex.

**19. ALL:** Shikamoo?

**20. DR FENTON:** Sawa, gari yangu hii hapa. Je mko tayari? Maana sina muda mwingi, lakini nataka kuwaonyesha kitu kimoja. Itatuchukua muda wa dakika 10 hivi kufika mahali tunakokwenda -nje kidogo ya mji.

**SFX:** **CAR DOORS OPENING, CLOSING, CAR DRIVING OFF**

**Scene Three: Outside a Cement Production Factory**

**SFX:** **CAR PULLING UP, ENGINE OFF, CAR DOORS OPENING**

**SFX ATMOS:** **CEMENT FACTORY**

**21. DR FENTON:** Kwa hivyo mlitaka kujua sababu kubwa za mabadiliko ya hali ya hewa. Sawa, kiwanda hiki cha saruji ni moja wapo ya viwanda vinavyochangia pakubwa mabadiliko ya hali ya hewa.

**22. ALEX:** Nini? Kiwanda kinachotengeneza saruji?

**23. DR FENTON:** Kuna awamu mbali mbali katika utengenezaji wa saruji. Na kila awamu inaathiri mazingira kwa kiwango kikubwa.

**24. CAROL:** Ni kiwanda kikubwa sana, na hata hakionekani kujali mazingira!

**25. DR FENTON:** Kwanza kabisa kiwanda hiki kinachafua mazingira kupitia vumbi angani, kisha kuna kelele na mitetemeko inayotokana na mashini zile unazoziona wakati zinapofanya kazi ya kupasua miamba, bila ya kusahau kalele zinazosikika wakati miamba inapolipuliwa.

**26. JOSHUA:** Kwa hivyo kelele zinaweza pia kuchafua mazingira?

**27. DR FENTON:** Hasa. Sisi wanasayansi wa masuala ya mazingira hupima aina zote za uchafuzi wa mazingira. Lakini aina ya uchafuzi inayotutia wasiwasi zaidi kutoka viwanda vya saruji ni utoaji wa gesi za viwandani.

**28. CAROL:** Ahh, mhalifu mwengine wa uchafuzi wa mazingira kupita gesi za viwandani!

**29. DR FENTON:** Ndiyo, hiyo ni kweli, Carol. Kiwanda hiki hutumia kiwango kikubwa cha makaa ya mawe kuchoma tanuru unayoiona pale kufikia viwango vikubwa vya joto kisha mawingu ya gesi ya dioksidi ya kaboni hutolewa. Haya yote ni kabla ya gesi zaidi kutolewa kutoka kwa malighafi nyengine zinazotumiwa katika mchakato mzima. Nafikiri utengenezaji wa saruji hutoa kiwango kikubwa zaidi cha gesi ya kaboni kuliko mchakato wowote wa kiviwanda

**30. ALEX:** Hizo si habari njema kamwe!

**31. DR FENTON:** Hapana! Si habari njema kabisa. Hasa ukikumbuka kwamba saruji huenda ni bidhaa ya pili inayotumika sana ulimwenguni baada ya maji.

**32. LORNA:** Nadhani kuna mahitaji makubwa ya saruji kwa ujenzi wa shule, hospitali, mabomba ya maji taka…..

**33. CAROL:** …….na hata vivanda vya kuzalisha umeme!

**34. DR FENTON:** Ehh na orodha ni ndefu mno!

**5. JOSHUA:** Lakini kama huwezi kuzuia watu kutumia saruji, utapunguza vipi uharibifu wa mazingira unaoongeza kwa kasi kubwa mabadiliko haya ya hali ya hewa?

**36. DR FENTON:** Ehhee, Hapa kuna njia mbili. Kwanza kabisa viwanda vya saruji vinapasa kuchukua hatua madhubuti kupunguza utoaji wa gesi inayochafua mazingira**.**

**37. JOSHUA:** Lakini hilo litawezekanaje, Dkt Fenton?

**40. DR FENTON:** Joshua, kinadharia viwadna vya saruji vinaweza kuweka vifaa vinavyoweza kunasa dioksidi ya kaboni. Kwa kufanya hivyo vitapunguza dioksidi hiyo ya kaboni kuingia hewani. Mpango huu unajulikana kama hifadhi ya kaboni, na teknolojia hii bado haijaimarishwa. Dioksidi ya kaboni inaweza kuhifadhiwa katika machimbo ya zamani ya mafuta au gesi. Lakini unahitaji kiwango kikubwa cha nishati kunyonya kaboni yenyewe na pia kuhakikisha kuwa inahifadhiwa kwa usalama mamia ya miaka katika ***mahodhi*** au mabwawa.

**41. LORNA:** Lakini kwa wakati huu hiyo itakuwa na maana utoaji wa gesi za viwandani utapungua na kupunguza kasi ya mabadiliko ya hali ya hewa. Inaeleweka! Inaingia akilini!

**42. DR FENTON:** Pili, tunapaswa kwa haraka kutafuta vyanzo mbadala vya nishati inayoweza kutumiwa tena na tena kwa ajili ya viwanda hivi. Kwa mfano kiwanda hiki cha saruji kinaweza kutumia nishati inayotokana na mvuke wa taka kuchoma tanuru badala ya kutumia makaa ya mawe.

**43. CAROL:** Vyanzo vya nishati inayoweza kutumiwa tena na tena? Nimesoma kuhusu aina hii ya nishati kwenye gazeti ninaloliuza kila siku. Nishati inayotokana na mimea, taka mmmm

**44. DR FENTON:** Ni kweli kabisa, lakini hiyo ni mada unayopaswa kuifanyia utafiti kando. Nishati inayotumika tena na tena na inayozingatia usafi wa mazingira ni mbinu mpya - hasa wakati huu ambapo kiwango cha mafuta kinapungua na pia kuwepo haja ya kuzuia mabadiliko ya hali ya hewa.

**45. LORNA:** Ni nani tunayeweza kuzungumza naye kuhusu aina hizi mpya z nishati zinazoweza kutumika tena na tena? Kwa hakika hilo ndilo litakalokuwa suluhisho kwa kiwanda hiki cha umeme kilichopendekezwa kujengwa!

**46. DR FENTON:** Nadhani namfahamu mtu mmoja, lakini muda wangu umekwisha nahitaji kurejea kazini. Kama mnavyoona kuna mambo mengi ya kufanya. Ingieni ndani ya gari nitawapa lifti hadi kituoni. Sawa?

**SFX:** **CAR DOOR CLOSING, CAR DRIVING OFF**

**Scene Four: Outside in the street**

**SFX ATMO:** **STREET MARKET**

**47. CAROL:** Soma! Soma kuhusu masuala yote…Hali mbaya ya hewa inakaribia! Onyo kuhusu kimbunga! Soma haya yote katika gazeti hili.

**48. PASSER-BY:** Kimbunga? Hebu nipe nakala moja tafadhali.

| | |
|---|---|
| **49. CAROL:** | Sawa hii hapa, ni senti 50 tu… Asante! **(taking money, handing over newspaper)**. Pia unaweza kutia saini ombi hili? Hili ni ombi la haki, kupinga ujenzi wa kiwanda kipya cha umeme hapa jijini. Unajua kiwanda hiki kitachangia pakubwa uharibifu wa mazingira na kuchangia ongezeko la joto duniani. |
| **50. PASSER-BY:** | Sawa, una kalamu? Mji huu hauhitaji kiwanda kikubwa cha umeme kitakachotoa moshi na gesi zinazochafua mazingira. Naomba unipe vipeperushi niwapelekee marafiki zangu pia! |
| **51. CAROL**: | Hilo litakuwa jambo la maana sana. Asante sana bwana, na tafadhali uendelee kusambaza ujumbe huu. …yaani "Kiwanda kinachozingatia usafi wa mazingira au bila kiwanda hicho kabisa!" |
| **SFX:** | **FOOTSTEPS, OVERTURNING OF TABLE** |

**52. CAROL:** Acha! Unafanya nini? Hayo ni makaratasi yangu! Huwezi kufanya hivyo!

**53. HEAVY:** Acha kuueneza habari za uongo.

**54. CAROL:** Sifahamu unachokizungumzia?

**55. HEAVY:** Kiwanda cha umeme kitajengwa na hakuna kundi lolote la wanafunzi litakaloweza kusimamisha ujenzi huo. Unasikia? Usijaribu kuchokoza nyuki au sivyo utapata hasara kubwa kuliko kupoteza hayo magazeti.

**SFX:** **STRIKING OF MATCH – FLAMES**

**56. CAROL:** Waaaacha ! Hizi ni pesa za kazi yangu ya siku **(crying)**. Unayateketeza…!

**57. PASSER-BY**: Ondoka hapa haraka kabla pia wewe sijakuteketeza. Kwanza yule mvulana ni nani?

**58. CAROL:** **(sobbing)** Simjui, lakini nadhani anataka kunitisha na rafiki zangu..

**59. PASSER-BY** Ana kibarua kigumu. Hata hivyo sina hakika kama nataka kuonekana na vipeperushi hivi vyako ikiwa in amaana watu kama yeye wataniandama. Pole sana mpenzi!

**60. CAROL:** **(sobbing)** Sasa tutafanyaje?

**END OF EPISODE 4**

**Outro:**

Na ni hayo tu tuliyoweza kuwaandalia kwa leo katika kipindi hiki cha Noa Bongo jenga Maisha yako. Mchezo huu kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa umeandikwa na Victoria Averill. Nikitumai utaungana nasi tena usikie Carol atachuku ahatua gani. Je atatupilia mbali juhudi zake baada ya vitisho hivi au atajipiga konde kifua na kusonga mbele na kampeini yake? Kumbuka ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki unaweza kutembelea mtandao wetu wa d w-world.d e /l b e Hadi wakati huo kwaheri kwa sasa na asante kwa kutusikiliza!